**MERCHANT SHIPPING NOTICE**
**MSN 1209**

**Rejeo 2/2022**

# MAELEKEZO JUU YA UTARATIBU WA VYOMBO KUANZA SAFARI ILI KUZUIA AJALI NA KUTOA HUDUMA ZA UTAFUTAJI NA UOKOAJI

**Tangazo hili linatolewa kwa Wamiliki wa vyombo vya majini, waendesha vyombo, Wamiliki wa Bandari na Mialo.**

**Tangazo hili lisomwe pamoja na Tangazo 'MSN 0407 Clearance of Vessels for Local Voyages and Reporting to Signal Stations When Entering or Leaving Ports'.**

## 1.0. Utangulizi

1.1. Kuna aina kadhaa za vyombo vinavyofanya shughuli katika maji ya Tanzania ambavyo ni pamoja na vyombo vya mizigo, abiria, uvuvi, shughuli maalum za kibandari uwekaji wa nyaya au mabomba baharini, upelekaji wa vifaa sehemu za utafutaji au uchimbaji wa mafuta na gesi majini (supply vessels), n.k.

1.2. Ni wajibu wa kila mwenye chombo kuhakikisha kuwa chombo chake ni salama kabla ya kuanza safari na kinatumiwa kwa matumizi yaliyokubalika na kuonyeshwa katika cheti cha ubora.

1.3. Ni wajibu wa kila chombo cha mizigo au abiria kutumia bandari au mwalo wenye usimamizi wa mmiliki au Serikali ya Mtaa wa eneo hilo au Beach Management Unit (BMU).

1.4. Chombo kitahesabiwa kuwa ni salama kama:

1.4.1 Kimekaguliwa na kukutwa kinakidhi matakwa ya viwango vya ubora vilivyowekwa na kina cheti cha ubora kinachostahili kilichotolewa na TASAC;

1.4.2 Kimebeba watu wasiozidi idadi inayoonyeshwa kwenye cheti cha ubora kwa kuzingatia idadi ya vifaa vya kuokolea maisha vilivyomo ndani ya chombo;

1.4.3 Kinaendeshwa na wafanyakazi wenye sifa zinazostahili; na

1.4.4 Kwa kuongeza, chombo cha mizigo kimepakiwa bila kuzidi uzito wa mizigo unaooneshwa kwenye cheti cha ubora au bila kuzamisha mstari uliowekwa kwenye chombo unaoonesha ukomo wa kupakia (load line) na kwa chombo cha abiria kimembeba abiria bila kuzidi idadi inayooneshwa kwenye cheti cha ubora.

1.5. Ni wajibu wa mmiliki au mwendeshaji (operator) wa chombo kuhakikisha kuwa, kabla ya abiria kupewa tiketi au ruhusa ya kupanda kwenye chombo kwa ajili ya kwenda safari amepata maelezo binafsi ya abiria huyo. Maelezo hayo yatakayothibitishwa na kitambulisho yatakuwa na taarifa zifuatazo za abiria:

1.5.1 Jina kamili;

1.5.2 Umri au mwaka wa kuzaliwa; na

1.5.3 Anwani ya posta au mahali anapoishi au mahali alipozaliwa.

1.6. Kwa mujibu wa kifungu 245 (4) cha Sheria ya Usafiri wa Majini ya Mwaka 2003, kuzidisha abiria ndani ya chombo ni kosa kwa mmiliki na nahodha wa chombo ambalo adhabu yake ni faini ya shilingi za Kitanzania sawa na dola za Kimarekani elfu tano au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kifungo na faini kwa pamoja.

1.7. Kwa mujibu wa kifunfu 255 (2) cha Sheria ya Usafiri wa Majini ya Mwaka 2003, chombo kupakia mizigo kuzidi

uzito unaoonyeshwa kwenye cheti cha ubora au kuzamisha mstari unaoonesha ukomo wa kupakia ni kosa kwa mmiliki na nahodha wa chombo ambalo adhabu yake ni faini ya shilingi za Kitanzania sawa na dola za Kimarekani elfu mbili au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili.

1.8. Kwa mujibu wa kifungu 255 (4) cha Sheria ya Usafiri wa Majini ya Mwaka 2003, kuanzisha safari chombo kilichopakia mizigo kuzidi uzito unaooneshwa kwenye cheti cha ubora au kuzamisha mstari unaoonesha ukomo wa kupakia ni kosa kwa nahodha wa chombo au mtu mwingine atakayehusika ambalo adhabu yake ni faini ya shilingi za Kitanzania sawa na dola za Kimarekani elfu ishirini au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kifungo na faini kwa pamoja.

1.9. Kwa mujibu wa kifungu 245 (2) cha Sheria ya Usafiri wa Majini ya Mwaka 2003 kupeleka safarini chombo ambacho hakina cheti cha ubora ni kosa ambalo adhabu yake ni faini ya shilingi za Kitanzania sawa na dola za Kimarekani elfu mbili au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kifungo na faini kwa pamoja.

## 2.0 Mambo Muhimu ya Kuzingatia Kabla ya Chombo kutoka Bandarini

2.1. Ni wajibu wa kila nahodha wa chombo cha mizigo au abiria kujaza fomu za ruhusa ya kutoka bandarini na kuziwasilisha kwa mhusika wa bandari au mwalo kabla ya kuanza safari. Fomu hizo zitasainiwa na nahodha wa chombo na ofisa mhusika wa bandari au mwalo na na ofisa mhusika huyo kubaki na nakala.

2.2. Ni wajibu wa mmiliki au msimamizi wa bandari kutoa ruhusa ya kutoka bandarini kuanza safari kwa chombo chochote cha mizigo au abiria kinachofanya safari katika mwambao wa Tanzania au maziwa, isipokuwa kivuko,

baada ya kuhakikisha kuwa kimejaza fomu za ruhusa ya kuondoka bandarini kama inavyostahili.

2.3. Ni wajibu wa kila mmiliki wa kivuko kuhesabu na kuhakikisha kuwa kivuko kinabebea idadi ya abiria na mizigo iliyoruhusiwa bila kuzidisha. Kumbukumbu za idadi ya abiria na mizigo kwa kila safari itatunzwa na msimamizi wa kivuko kwa muda usiopungua miezi sita.

## 3.0 Vifaa na Mpango wa Kutoa Huduma ya Utafutaji na Uokoaji

3.1. Pamoja na hatua zinazochukuliwa kuzuia ajali, bado kuna uwezekano wa ajali kutokea na huduma ya utafutaji na uokoaji kuhitajika.

3.2. Ni wajibu wa mmiliki au mwendesha bandari au mwalo kuwa na vyombo na/au mpango wa utafutaji na uokoaji. Mpango huo utawezesha bandari au mwalo husika kutoa msaada kwa chombo kilicho katika janga ndani au karibu na bandari au mwalo huo ili kuokoa maisha ya watu.

## 4.0 Taarifa Zaidi

Msajili wa Meli
Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)
Ghorofa ya 8 PSSSF TOWER, Mtaa wa Ohio / Garden
S.L.P 989
Dar es Salaam
Tanzania
Simu +255 222 127 314
Nukushi +255 222 127 313
Barua pepe: dg@tasac.go.tz, info@tasac.go.tz
Tovuti: www.tasac.go.tz